MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 12/11/2021

MAHUDHURIO:

1. Bw. Fredrick K. Juma - Mwenyekiti
2. Bw. Damian Morice Ogila - Katibu
3. Patrice M. Boniphace - Mjumbe
4. Bi. Monica A. Magutu - Mjumbe
5. Bw. Haruna Matata - Mwanasheria

WAJUMBE WASIOHUDHURIA:

Bw. Charles Moremi

SEKRETARIETI:

1. Mnubi Chausiku - Afisa Ugavi
2. Maria P.Machugu – Afisa Ugavi
3. Imelda A.Magaria – Afisa Ugavi msaidizi

AJENDA

1. Kufungua kikao
2. Kupitia na kuthibitisha ajenda
3. Kusoma na kuthibitisha muhtasari wa kikao kilichopita
4. Taarifa ya utekelezaji wa Maazimio ya kikao cha tarehe 15/10/2021
5. Kujadili na kuidhinisha manunuzi yaliyofanywa kwa njia ya mzunguko (Circular resolution)
   (i) Kuidhinisha tangazo la zabuni ya kukodisha jengo la biashara lililoko kiwanja Na.6 Block E
   (ii) Kuidhinisha ununuzi wa mafuta lita 3000 Tzs 7,353,000/= idara ya Mipango
   (iii) Kuidhinisha ununuzi wa shajala kiasi cha Tzs 3,990,000/= idara ya Mipango
   (iv) Kuidhinisha ununuzi wa mafuta idara ya Utawala ya Tzs 4,902,200/=
6. Kujadili na kuidhinisha manunuzi ya miradi ya Maendeleo kwa ustawi wa Taifa na mapambano ya UVIKO 19
7. Kujadili na kuidhinisha manunuzi ya dawa na vifaa tiba kutoka bohari ya dawa (MSD) yenye thamani ya Tzs.10,957,723.79
8. Kujadili na kuidhinisha Mzabuni wa ulinzi baada ya majadiliano
9. Kujadili na kutoa idhini ya manunuzi ya dawa yaliyokosekana MSD kwa njia ya kotesheni
10. Kufunga kikao

Scanned with CamScanner

**MUH NA.HMT/BZ/12/11/2021/1: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti wa Bodi ya zabuni alifungua kikao mnamo saa 5:15 Asubuhi akiwakaribisha wajumbe kujadili ajenda zilizoletwa.

**MUH NA.HMT/BZ/12/11/2021/2: KUPITIA NA KUTHIBITISHA AJENDA**

Ajenda zilipitiwa na zote kuthibitishwa kuendelea kujadiliwa.

**MUH NA.HMT/BZ/12/11/2021/3: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO KILICHOPITA CHA TAREHE 15/10/2021**

Katibu wa bodi aliwasomea wajumbe muhtasari wa kikao cha tarehe 15/10/2021.Wajumbe waliridhia kuwa yaliyomo kwenye muhtasari ndiyo yaliyojadiliwa.Muhtasari ulithibitishwa.

**MUH NA.HMT/BZ/12/11/2021/4: TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 15/10/2021**

Katika kikao cha tarehe 15/10/2021 Bodi ya zabuni ilitoa maazimio kuhusu kutuza zabuni ya Ujenzi wa soko la kisasa kwa Kampuni ya Mohammedi Builders Ltd kwa kuelekeza Mkandarasi mshauri wa mradi (Mhandisi Consultant Ltd) kupunguza kiasi cha kazi (Rescoping) katika mradi wa ujenzi wa soko.

Bodi ya zabuni ilitoa ushauri kwa Uongozi wa Halmashauri kuomba msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) katika vifaa vya ujenzi wa soko la kisasa ili kupunguza gharama ya mradi.

Akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa maazimio hayo,Katibu wa Bodi aliwajulisha wajumbe kuwa Mshauri mwelekezi wa mradi wa ujenzi wa soko alipitia vipengele vya mradi na kupunguza kipengele cha Fedha za tahadhari (Contingency) kutoka 5% ya awali na kuwa 2.5%. Kwa kufanya hivyo bei ya Zabuni imekuwa ni Tzs 9,511,254,574.99 ikiwemo Kodi ya ongezeko la thamani ya Tzs 1,450,869,341.95. Bodi ya Zabuni iliridhia Mkandarasi Mohammedi Builders Ltd kupewa kazi hiyo.

**MUH NA.HMT/BZ/12/11/2021/5: KUJADILI NA KUIDHINISHA MANUNUZI YALIYOFANYWA KWA NJIA YA MZUNGUKO (CIRCULAR RESOLUTION)**

Katibu wa bodi ya zabuni aliwajulisha wajumbe kuwa ofisi ya Ugavi ilipokea maombi ya manunuzi ya idara mbalimbali yaliyopitishwa kwa njia ya "Cicular resolution" na kushauri yaidhinishwe kwa mujibu wa sheria na taratibu. Manunuzi hayo ni kama ifuatavyo:- (a)Kuidhinisha tangazo la zabuni ya kukodisha jengo la biashara lililoko kiwanja Na.6 Block E

(b)Kuidhinisha ununuzi wa mafuta lita 3000 Tzs 7,353,000/= idara ya Mipango
(c)Kuidhinisha ununuzi wa shajala kiasi cha Tzs 3,990,000/= idara ya Mipango
(d)Kuidhinisha ununuzi wa mafuta idara ya Utawala ya Tzs 4,902,200/=

AZIMIO :Bodi ya zabuni iliidhinisha manunuzi hayo

Scanned with CamScanner

**MUH NA.HMT/BZ/12/11/2021/6: KUJADILI NA KUIDHINISHA MANUNUZI YA MIRADI YA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO YA UVIKO 19**

Katibu aliwajulishe wajumbe kuwa shule 12 za Halmashuri ya Tarime Mji zilipokea fedha za miradi ya ujenzi wa madarasa 32 ambapo njia mojawapo iliyoelekezwa kufanya manunuzi ni "Single source"

Baada ya kuwasilisha nukuu mbalimbali za bei ya vifaa vya ujenzi wazabuni wafuatao walipitishwa:-

| S/N | JINA LA KAMPUNI | AINA YA VIFAA VYA UJENZI |
|---|---|---|
| 1 | Edward John Makanya/Joseph Chacha | Matofali ya saruji |
| 2 | John Kirongochi Marwa/Mseti Heche Suguta | Saruji |
| 3 | Mama Leah Hardware/Tarime Hardware/Chrispinus M.Mukohi/Jura (T) Ltd | Bidhaa mbalimbali za Viwandani |
| 4 | Kinyambi Gen.Supply/Wambura Mchuma/Mama Leah Hardware/Michael N.Gesase/Stephano D.Wangwe/ | Madini ujenzi (Mawe,Kokoto,Mchanga,Kifusi) |
| 5 | Gaini Co.Ltd/Tarime Hardware | Nondo 12mm,8mm ,Misumari |
| 6 | ALAF LTD | Mabati 28 G ,MT 3 |
| 7 | Godson Musa Msisi/Kinyambi Gen.Supply/Chrispinus M.Mukohi/Nyamhanga B.Nyangige | Mbao aina mbalimbali |
| 8 | Kiboko Paints (T) Ltd/Mama Leah/Chrispinus M.Mukohi | Rangi za ujenzi |
| 9 | Bageni Patrick/Mama Leah Hardware | Shutter za milango/Fremu za milango |
| 10 | Netto S.Joseph/Omari Kiwali/Francisko Rolex | Madirisha ya grill na vioo |
| | | |

**MUH NA.HMT/BZ/12/11/2021/7: KUJADILI NA KUIDHINISHA MANUNUZI YA DAWA NA VIFAA TIBA KUTOKA BOHARI YA DAWA (MSD) YENYE THAMANI ya Tzs.10,957,723.79**

Katibu wa Bodi aliwaeleza wajumbe kuwa ofisi ya Ugavi ilipokea maombi ya manunuzi ya dawa na vifaa tiba kutoka idara ya Afya yenye thamani ya Tzs 10,957,723.79 na kuomba idhini ya manunuzi hayo.

AZIMIO:

Wajumbe wa Bodi ya zabuni waliidhinisha manunuzi yafanyike kutoka Bohari ya dawa (MSD)

**MUH NA.HMT/BZ/12/11/2021/8: KUJADILI NA KUIDHINISHA MZABUNI WA ULINZI BAADA YA MAJADILIANO**

Scanned with CamScanner

Taarifa ya timu ya majadiliano ya zabuni ya ulinzi ilisomwa mbele ya wajumbe.Katika majadiliano hayo makubaliano yalifikiwa ambapo Kampuni ya ulinzi ya SUMA JKT GUARD LTD imeridhia Malipo ya Ulinzi kwa gharama ya Tzs 5,120,000/= kwa mwezi pamoja na VAT.

AZIMIO:

Bodi ya zabuni imeidhinisha Kampuni ya SUMA JKT GUARD LTD kuingia Mkataba wa ulinzi na Halmashauri ya Mji Tarime.

**MUH NA.HMT/BZ/12/11/2021/9: KUJADILI NA KUTOA IDHINI YA MANUNUZI YA DAWA YALIYOKOSEKANA MSD KWA NJIA YA KOTESHENI**

Katibu aliwajulisha wajumbe juu ya maombi kutoka idara ya afya ya kununua dawa zilizokosekana bohari ya serikali (MSD) ambapo taratibu zinaruhusu dawa zilizokosekana MSD kununuliwa kwenye maduka ya kawaida ya dawa (Pharmacy). Wajumbe walijadili hoja hiyo na kutoa azimio.

AZIMIO:

Kotesheni ya bei ya dawa zisambazwe katika maduka mbalimbali ya dawa ili kupata muuzaji mwenye bei nafuu.

**MUH NA.HMT/BZ/12/11/2021/10: KUFUNGA KIKAO**

Mwenyekiti wa Bodi alifunga kikao majira ya saa 7 mchana kwa kuwashukuru wajumbe waliohudhuria.

Umesainiwa tarehe 28/1/2022

| | |
|---|---|
| Fredrick K. Juma | Damian Morice Ogila |
| Saini ............................ | Saini.............................. |
| Mwenyekiti | Katibu |

Scanned with CamScanner